**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKINOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE:**
**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU,**
**S. L. P 27,**
**TUKUYU.**

**Kumb. Na.TSS/JI/VOL.II/11TAREHE ----------**

**Namba za simu:**
**Mkuu wa shule;0753695250**
**Makamu mkuuwa shule: 0763455191**
**Mwandamizi malezi: 0766758758**

**KWA** ----------
---
---
---

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO (V) KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano (**V**) mchepuo/Tahasusi _____ mwaka wa masomo _____, shule itafunguliwa tarehe_____**/07/2021** na wewe utatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe **_____/07/2021 pasipo kuchelewa.**

**MAHALI SHULE ILIPO:**
Shule ya sekondari Tukuyu ni ya Serikali, shule hii iko Mkoani Mbeya,Wilaya ya Rungwe. Shule hii ipo Tukuyu Mjini, mkono wa kushoto katika barabara iendayo Kyela. (Mita 150 kutoka stendi kuu, mwendo wa dakika tano(5) kwa miguu)

**MAAGIZO:**
**1: 1 WAVULANA (SARE)**

- Suruali tatu (3), (i) Moja rangi nyeusi kitambaa cha tetron na tai yake ndefu
  (ii) ya pili rangi ya…….**angalia kiambata** na tai yake ndefu(**anaweza akashonea shuleni**)
  (iii) ya tatu rangi ya kahawia/ugoro **(shamba dress)**

  **NB:** Utatakiwa uje na suruali zote tatu zilizoshonwa vizuri na zenye mifuko mitatu, marinda**(celebrations)** upana miguuni usiopungua inchi kumi na saba **(17),** hatutahitaji suruali zilizoshonwa mtindo wa jeans. Aina ya kitambaa angalia kiambatanisho.**Ili kuweka kipimo sawa cha sare, mwanafunzi anashauriwa aje na fedha ili ashone akiwa shuleni.**
- Mwanafunzi aje na shati mbili rangi nyeupe mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu.
- Soksi ndefu nyeupe.
- Sweta ya rangi ya kijani kibichi shingo yake iwe na umbo la **V**

- Alete Mopa na brashi ngumu moja **(1)** na Ndoo kubwa moja **(1)** ya plastiki ya lita 20.
- Aje na Godoro futi mbili na nusu **(2.5)** kwa sita **(6).**
- Aje na shuka jozi mbili **(2)** moja rangi ya pinki na moja rangi ya bluu bahari.
- Aje na blanketi zito la kutosha kujisitili kipindi cha baridi.
- Aje na mto mkubwa wa kulalia mmoja**(1)** na foronya mbili **(2)**
- Aje na chandarua ili kujikinga na mbu.
- Aje na taulo mbili.
- Aje na mswaki, dawa ya meno, sabuni za kutosha na kandambili jozi moja **(1).**
- Aje na shilingi 15, 000/= tasilimu kwa ajili ya T-shirt itakayovaliwa nje na muda wa darasani.
- Aje na ream moja **(1)** ya karatasi **A4**.
- **Nguo za nyumbani haziruhusiwi.**
- **Simu haziruhusiwi shuleni.**

**1:2 WASICHANA (SARE)**

- Sketi tatu (03),
  (i) moja rangi nyeusi
  (ii) ya pili rangi ya …….**angalia kiambata ( Anaweza akashonea shuleni )**
  (iii) ya tatu yangi ya kahawia/ugoro (shamba dress)
  **NB:**Unatakiwa uje na sketi mbili zilizoshonwa vizuri na zenye marinda na ndefu zinazokaribia visigino, **hatutahitaji sketi fupi.**
  Aina ya kitambaa angalia kiambatanisho.**Ili kuweka kipimo sawa cha sare, mwanafunzi anashauriwa aje na fedha ili ashone akiwa shuleni.**
- Aje na blauzi mbili **(2**) rangi nyeupe zenye mikono mirefu
- Aje na viatu vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu.
- Soksi nyeupe ndefu jozi tatu **(3).**
- Sweta rangi ya kijani kibichi shingo yake iwe na umbo la **V**
- Alete Mopa na brashi ngumu moja **(1)** na ndoo kubwa moja **(1)** ya plastiki ya lita 20.
- Watakao hitaji kuvaa hijabu wanatakiwa kuvaa sketi ndefu inayotosha kusitiri mwili wa atakaye vaa.
- Aje na Godoro futi mili na nusu **(2.5)** kwa sita **(6).**
- Aje na shuka jozi mbili **(2),** moja rangi ya pinki na moja rangi ya bluu bahari.
- Aje na blanketi zito la kutosha kujisitili kipindi cha baridi.
- Aje na mto mkubwa mmoja **(1)** na foronya mbili **(2).**
- Aje na chandarua ili kujikinga na mbu.
- Aje na taulo mbili.
- Aje na mswaki, dawa ya meno, sabuni za kutosha na kandambili jozi moja **(1).**
- Aje na shilingi 15,000/= tasilimu kwa ajili ya T-shirt itakayo valiwa nje na muda wa darasani (masomo)
- Aje na ream moja **(1)** ya karatasi **A4.**
- **Nguo za nyumbani haziruhusiwi.**
- **Simu haziruhusiwi shuleni.**

**NB:**

- Suruali/Sketi ya rangi nyeusi itavaliwa siku ya Jumatatu hadi Jumatano.
- Suruali/Sketi ya rangi ya brown itavaliwa siku ya Alhamisi hadi Ijumaa.
- Suruali/Sketi ya rangi ya kahawia/ugoro pamoja na T-shirt zitavaliwa nje na muda wa darasani.
- Mwanafunzi anapokwenda kuabudu (Kanisani/Msikitini) atatakiwa kuvaa sare za shule kama kawaida na si vinginevyo.

**1:3 VIFAA VYA MICHEZO:**

**WAVULANA:**

(a) Bukta moja **(1)** na Track suti nyeusi yenye ufito mweupe.
(b) Raba jozi moja **(1).**
(c) Fulana (T-shirt) rangi nyekundu isiyo na maandishi, kolana yenye mikono mifupi.
(d) Soksi jozi moja **(1)** ziwe ndefu.

**WASICHANA:**

(a) Bukta moja **(1)**na track suti nyeusi yenye ufito mweupe.
(b) Raba jozi moja **(1).**
(c) Kigauni rangi ya blue.
(d) Soksi jozi moja **(1)** ziwe ndefu.
(e) Fulana (T-shirt) rangi nyekundu isiyo na maandishi,kolana yenye mikono mifupi.

**NB:** Zingatia maagizo ya mavazi, nguo zingine za nyumbani hazihitajiki.

**1:4 VIFAA VYA MASOMO:**

Unatakiwa kuja/ kuleta vifaa vya masomokama ifuatavyo:-

- Madaftari makubwa (counter books) angalau kumi**(10) (ukubwa wa 4 quires)** kwa ajili ya masomo yote utakayosoma .
- Kalamu za kutosha za wino mweusi au bluu na za risasi.
- Mkebe wa hisabati (mathematical set).
- Mwanafunzi wa mchepuo wa sayansi anatakiwa kuja na koti jeupe refu kwa ajili ya kuvaa anapoingia maabara kujifunza kwa vitendo. **(Practical studies)**
- Aje na "scientific calculator"
- Aidha mwanafunzi wa mchepuo wa **PCB** anatakiwa kununua **"dissection kit"** kwa ajili ya mazoezi awapo shuleni**. ( ATAITUNZA MWENYEWE )**
- **Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu vya masomo ya tahasusi aliyopangiwa/aliyochaguliwa.**

**1:5 ADA NA MICHANGO MINGINE:**

(i) Ada ya shule kwa wanafunzi wa bweni ni shs. **70,000/=** kwa mwaka , yaani shs. **35, 000/=**kwa kila mhula.
(ii) Fedha ya tahadhari shs sh. **5,000/=**
(iii) Fedha ya kitambulisho sh. **6,000/=**
(iv) Ukarabati wa samani sh. **15, 000/=**
(v)Fedha ya taaluma sh. **20,000/=**
(vi)Fedha ya kulipa walinzi, wapishi na vibarua wengine sh. **30, 000/=**
(vii)Fedha ya ujenzi sh. **30,000/=**
(viii)Kwa yule ambaye hana Bima ya Afya alete sh. **10,000/=**kwa ajili ya kukatiwa Bima kwa miaka miwili (2) takayo kuwepo shuleni.
(ix)Nembo ya shule sh. **2,000/=**

**NB:** Fedha hizo za ada na michango mingine zinatakiwa zipelekwe Benki (NMB)kwenye Account **No. 61403500086 JINA :TUKUYU SECONDARY.**Mwanafunzi anatakiwa alete **"pay in Slip"** Shuleni baada ya kutoa nakala (Photocopy).

**1:6 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABLA YA KUFIKA SHULE:**

(i) Mwanafunzi apimwe na daktari wa Hospitali ya Serikali. Tumia fomu iliyoambatanishwa.
(ii) Kuleta cheti cha kuzaliwa (nakala) au "affidavity" ambayo hupatikana mahakama ya Wilaya. Mzazi/mlezi amabaye mtoto wake hana cheti cha kuzaliwa unatakiwa uende na fomu hii pamoja na mtoto wako Mahakamani kwa kiapo.
(iii) Kusoma na kuzielewa Sheria/Kanuni za shule.
(iv) Jaza fomu ya maelekezo yanayohusika (taarifa binafsi).

(v) Kila mwanfunzi anatakiwa kuleta picha nne (4) za wazazi au Ndugu wa karibu wa mwanfunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni pamoja na namba zao za simu.

**2. CHAKULA:**

Huduma ya chakula itakuwepo, wanafunzi watapata chai, chakula cha mchana na jioni. Unapokuja uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya chakula:-

i) Sahani
ii) Kikombe
iii) Bakuli na
iv) Kijiko

Mwanafunzi yeyote hatahusika kupika chakula awapo shuleni.

**3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kufuata na kutekeleza sheria na kanuni zote za shule kama inavyotakiwa.
**NB:** soma kiambatanisho Na. 1

**4. KUSAJILIWA:**

Mwanafunzi anatakiwa kuonyesha **Leaving Certificate, Result slip, Bank pay in slip** na vifaa vingine anavyotakiwa kuwasilisha anaporipoti ndipo atapokelewa na kusajiliwa na si vinginevyo. Hivyo ni muhimu kuja na vitu hivyo.

Kumbuka kuwa wewe umebahatika kupata nafasi hii ya pekee kati ya maelfu ya wanafunzi waliofanya mtihani. Hivyo ni lazima kuitumia nafasi hii kwa faida yako na Taifa. Kinachokuleta katika shule hii, ni kujifunza na kuelimika. Hivyo unatakiwa kudumisha heshima na sifa ya shule hii ya Tukuyu.

**Unapofika ripoti kwa mwalimu wa zamu au ofisi ya malezi au makamu Mkuu wa Shule au Mkuu wa Shule hii ili upewe maelekezo zaidi.**

**Kiambata Na. 1**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**
**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya **Elimu Na. 25 ya mwaka 1978.** Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Wewe kama mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;-
   (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
   (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule ni muhimu.
   (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
   (d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na zingine utakazopewa.
   (e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
   (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule.
   (g) Kuvaa sare ya Shule wakati unapotakiwa.
   (h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.
   (i) Kutomiliki na kutumia **SIMU AU VIFAA VINAVYOHUSIANA NA SIMU( mfano: charger , line , betery la simu n.k)** katika mazingira ya Shule.
   (j) Kupita njia sahihi utokapo na uingiapo katika eneo la Shule kwa ruhusa (kibali) maalumu.

2. **Makosa yanayoweza kusababisha kuadhibiwa / ukafukuzwa Shule baadhi ni kama yafuatayo;-**
   (a) Wizi
   (b) Uasherati, ubakaji na ushoga.
   (c) Kufuga ndevu
   (d) Kusuka nywele kwa mtindo wowote ule uwapo shuleni.
   (e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
   (f) Uvutaji bangi.
   (g) Makosa ya jinai.
   (h) Kupiga au kupigana.
   (i) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
   (j) Kudharau bendera ya Taifa.
   (k) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya Shule.
   (l) Kutoa mimba.
   (m) Kugoma, kuchochea na kuongoza vurugu au kuvuruga amani na usalama wa Shule na watu.
   (n) Kukataa adhabu kwa makusudi.
   (o) Utoro wa vipindi na kutohudhuria masomo kwa muda wa siku tisini **(90)** mfululizo bila taarifa rasmi.
   (p) Kutofanya mazoezi, majaribio na mitihani mbalimbali bila sababu maalum.
   (q) **KUMILIKI NA KUTUMIA SIMU**, laini, chaja, na viashiria vinavyopelekea kuwa na Simu katika mazingira ya Shule.
   (r) Kupita njia zisizoruhusiwa kwa mujibu wa sheria wakati wa kutoka na kuingia katika eneo la shule na uwapo ndani ya Shule kwa mfano **KURUKA UKUTA/UZIO** wa Shule, **KURUKA DIRISHA**, n. k
   (s) Kuvaa mavazi yanayobana na milegezo.
   (t) Kutoka nje ya eneo la Shule bila kibali.
   (u) kumiliki / kukutwa na silaha au viashiria vya uvunjifu wa amani

**NI WAJIBU WA KILA MWANAFUNZI KUZINGATIA NA KUTII TARATIBU, KANUNI NA SHERIA ZA SHULE BILA KUSHURUTISHWA:**

**……..**
**MWAKIPUBA, F . A**
**(MKUU WA SHULE)**

**Kiambata Na.2**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA:**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

**PART A:**

To the medical Officer, From; ----------
---------- -------- ----------
---------- ----------
---------- ---------- Date; ----------

**Re:** _____

Please Examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Secondary School studies that may also include military training, the Examination should include the following categories **(I-IV)** each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnant category (**category IV**) will also render a girl candidate ineligible for the cause.

I. (a) Eye sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) General diseases
(e) Leprosy
(f) Epilepsy
(g) Limbs

Other serious disease ----------
Pregnancy ----------

**PART B: MEDICAL OFFICER:**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have Examined the above named and consider that he/she is physically fit for a full time Secondary school studies.

(a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) General diseases
(e) Leprosy
(f) Epilepsy

II. Neuroses ----------

III. Other serious diseases ----------

IV. Pregnancy ----------

**DATE ---------- SIGNATURE ----------**

**STATION ---------- DATE ----------**

**Kiambata Na.3**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKINOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**
**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:**

**SEHEMU A:**

1. Jina kamili la mwanafunzi ----------
2. Tarehe ya kuzaliwa ---------- kabila ----------
3. Jina la mzazi/mlezi ----------
4. Uhusiano ---------- kazi yake ----------
5. Anuani ya Mzazi/Mlezi ----------
6. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ----------
7. Umbali kuja Shuleni ni KM ----------
8. Majina ya Ndugu/Walezi wengine wa karibu;-

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU | MAHALI ALIPO |
|---|---|---|---|
| (i) | | | |
| (ii) | | | |
| (iii) | | | |
| (iv) | | | |

**TANIBIHI:** Wale wenye picha tu.

9. **MENGINEYO:**
   (Kama mgonjwa aje na uthibitisho wa daktari, kama ni yatima aje na hati ya kifo, kama ni mlemavu, n.k).
   ----------
   ----------

**SEHEMU B:**

**TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

Mimi ---------- (majina matatu) nimezisoma na kuzielewa Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule na kwamba niko tayari/ siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi ---------- Tarehe ----------

**SEHEMU C:**
**TAMKO / AHADI YA MZAZI/ MLEZI:**

Mimi ---------- ambaye ni Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi ---------- ninaahidi kwamba nitatekeleza / sitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya Shule kama nilivyoelekezwa na kwamba niko tayari / siko tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua taaluma na nidhamu yake. Pia ninakubali kutii Taratibu, Kanuni na sheria zote za shule na kulipa Ada na michango mingine kama ilivyoelezwa pia ntafuata maelekezo mengine kadri yatakavyotolewa na uongozi wa Shule ya Sekondari Tukuyu.

Sahihi ya Mzazi / Mlezi ---------- Tarehe ----------

**Kiambata na. 4**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE:**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

## TAMKO LA UTII WA SHERIA ZA SHULE:

Kwa kuheshimu agizo la **Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari Tukuyu** tarehe **30/03/2016** alilolitoa mbele ya wanafunzi wote pamoja na kuagiza kuwa wazazi wa wanafunzi waliofanya makosa ya utovu wa nidhamu thelathin na mbili **(32),** ambao wanafunzi kumi na saba **(17)** walisababisha vurugu, nane **(8)** hawakuhudhuria "roll call" ya usiku wa tarehe **05/03/2016**, wanne **(4)** kukamatwa na simu na watatu **(3)** kuruka ukuta/uzio wa shule kutoa tamko la kuwataka wanafunzi wote kutii na kuheshimu sheria zote za shule.

Nakuwa mwanafunzi yeyote atakaye kamatwa na Simu ama kifaa chochote kinachoashiria kumiliki Simu na kuruka ukuta/uzio (fence) wa shule pamoja na makosa mengine atakuwa kwa makusudi amejifukuza shule yeye mwenyewe tangu hapo.

## KIAPO CHA MWANAFUNZI:

Kuwa mimi mwnafunzi wa Shule ya Sekondari Tukuyu, nimekubali kuishi katika jumuiya hii nikiwa mtiifu na kufuata sheria zote za shule kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka1978** kama ilivyorekebishwa na **sheria Na. 10 ya mwaka 1995.**Bodi ya shule imepewa mamlaka ya kusimamia nidhamu ya wanafunzi. Hivyo, ninaahidi kufuata utaratibu wote ulioainishwa kwenye sheria za shule wakati wote ninapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Hivyo mimi---------- ( majina matatu) nikiwa mwanafunzi wa kidato cha ---------- katika Shule ya Sekondari Tukuyu ninaapa kutomiliki Simu ama kifaa chochote kinachoashiria kumiliki **Simu** pamoja na urukaji **uzio/ukuta** (fence) wa shule pia kutoshiriki mgomo , fujo au kuanzisha mgomo au fujo. Ninaahidi kuwa mtiifu na mwanafunzi mwenye adabu kwa walimu wangu wote na watumishi pamoja na wanafunzi wenzangu wa jumuiya ya Shule Sekondari Tukuyu ili niweze kufaulu masomo yangu vizuri.

Pia leo tarehe ---------- mwezi---------- mwaka---------- ninaahidi kuwa nikikamatwa na **Simu** ama kifaa chochote kinachoashiria mimi kumiliki simu na nimeruka **uzio/ukuta** (fence) wa shule pamoja na makosa mengine ambayo ni kinyume na Taratibu, Kanuni na Sheria za shule nifukuzwe shule kabisa.

Mimi ---------- (majina matatu).
Sahihi ---------- leo tarehe ----------

Mbele ya mkuu wa Shule ya Sekondari Tukuyu kwa niaba ya Bodi ya Shule ya Sekondari Tukuyu.

---------- **Mhuri wa ofisi**

**KATIBU WA BODI YA SHULE**

**Kiambata na. 5**

**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU**
**TAARIFA ZA NDUGU (WAZAZI/WALEZI) WA MWANAFUNZI WATAKAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI.**

1. JINA ……. ….
   JINSI ……..
   UHUSIANO ……..
   ANAKOTOKA……. ….
   ANUANI ……
   NA. YA SIMU ……

   Picha

2. JINA ……..
   JINSI ……..
   UHUSIANO ……..
   ANAKOTOKA ……..
   ANUANI ……
   NA. YA SIMU ……

   Picha

3. JINA ……. ….
   JINSI ……..
   UHUSIANO ……..
   ANAKOTOKA……. ….
   ANUANI ……
   NA. YA SIMU ……

   Picha

4. JINA ……..
   JINSI ……..
   UHUSIANO ……..
   ANAKOTOKA ……..
   ANUANI ……
   NA. YA SIMU ……

   Picha

Mimi …….. (Mwanafunzi) kidato cha ……kuanzia mwaka wa masomo …….. hadi …… Nathibitisha kuwa watajwa na wenye picha hapo juu ni Wazazi/Walaezi/Ndugu zangu watakaonitembelea muda wote nitakapokuwa katika shule hii ya Tukuyu Sekondari.

**Sahihi ……** **Tarehe ……..**